**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

**Simu:** Mkuu wa Shule 0754048835, M/Mkuu wa Shule 0757612107
Mwl. Malezi 0655678821
Email: iyungasecondary@gmail.com
Website: www.iyungatechnicalschool.sc.tz

**SHULE YA SEKONDARI IYUNGA**
**S.L.P. 701**
**MBEYA.**

***Unapojibu tafadhali taja:***
KUMB NA. IYU/U/12 06/12/2019

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
…………………………………..
S.L.P. ……………………………
……………………………………

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IYUNGA, HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, MKOA WA MBEYA KIDATO CHA KWANZA 2020**

**1. Utangulizi:-**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020.

Shule ya Sekondari Iyunga ipo umbali wa kilometa tano (5) Magharibi mwa jiji la Mbeya. Usafiri wa basi dogo (Hiace) kutoka kituo kikuu cha mabasi Mbeya unapatikana na nauli ni shilingi mia nne tu (400/=)

Muhula wa masomo unaanza tarehe 06/01/2020 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 05/01/2020.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare ya shule**

(a) Suruali mbili (2) rangi ya kaki inayofanana kama ya polisi, ya heshima siyo “modo” (iwe na marinda mawili).
(b) Mashati mawili rangi nyeupe mikono mifupi yote yawe marefu yakuweza kuchomekewa kwenye suruali.
(c) Tai nyeusi ndefu ya kufika kiunoni
(d) Viatu vya shule vyeusi vya ngozi jozi 2. Viwe vya heshima vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
(e) Soksi rangi nyeusi jozi mbili.
(f) Sweta rangi ya bluu (Rangi ya kizibo cha biki) shingo ya “V”
(g) Mkanda mweusi wa suruali usio na picha wala madoido.
(h) T-shirt mbili rangi ya kijivu, moja itatumika kama shamba dress na nyingine kwa ajili ya michezo.

(i) Vifaa vya michezo: raba/viatu vya michezo, Bukta rangi ya bluu, stokings (soksi) ndefu jozi mbili.
(j) Nguo za kushindia (shamba dress) ambazo ni Tracksuit mbili, rangi ya kijivu yenye miraba rangi nyeupe kuanzia kiunoni mpaka kwenye unyayo na kuanzia begani hadi kwenye kiganja ivaliwe wakati wote baada ya masomo.
(g) Overall rangi ya bluu kwaajili ya masomo ya ufundi

**2.2 Mahitaji muhimu**

(a) Godoro la futi 2.5
(b) Shuka za kujifunika 2 za light bluu
(c) Blanketi zito moja kwa ajili ya kurkaribiana na msimu wa baridi
(d) Taulo moja, mto mmoja
(e) Madaftari makubwa (counter books) 10 na ndogo 3.
(f) Rula, kalamu na penseli za kutosha
(g) Mswaki, sabuni, dawa ya meno na dawa ya viatu
(h) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
(i) Chandarua kwaajili ya kujikinga na mbu

**3. <u>MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:</u>**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kuwa na nywele ndefu. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
(xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xv) Kudharau alama za taifa yaani bendera yaTaifa,fedha, picha ya Rais,mwenge n.k.
(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
(xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
(xviii) Kugoma adhabu halali ya mwalimu au kiranja.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu:**

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

(e) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.

(f) Nakala ya result slip kutoka Necta.

**5. Maelekezo mengine muhimu**

(i).Mwanafunzi anatakiwa awe na nauli ya kurudia nyumbani wakati wa likizo.

(ii). Shule haitoi huduma ya chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa

**6. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Sahihi ya Mkuu wa Shule ……………………………………..**

**Jina la Mkuu wa Shule EDWARD J. MWANTIMWA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule …………………………………**

# SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

**UTANGULIZI:**
Kila mwanafunzi itampasa kufuata taratibu na kanuni za shule hii kama zilivyoonyeshwa hapo chini.
.

## TARATIBU ZA MASOMO

A. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shule inapofungua na kuzingatia mambo yafuatayo:-
   i. Kuingia darasani mapema kabla ya mwalimu
   ii. kusimama na kusalimu mwalimu anapoingia darasani
   iii. kuhudhuria vipindi vyote vilivyopangwa katika ratiba ya darasa lake.
   iv. Kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayomhusu
   v. Mwanafunzi atawajibika kujifunza na kuongea kiingereza muda wote awapo shuleni ikiwa ni pamoja na kutekeleza kanuni ya **SPEAK ENGLISH ONLY.**
   vi. Mwanafunzi anyooshe mkono wake juu na asimame wakati wa kuuliza au kujibu maswali.
   vii. Mwanafunzi akiwa hapa shuleni anatakiwa kuhudhuria maandalizi ya jioni (night preparations) bila kukosa. Vinginevyo adhabu kali itatolewa.
   viii. Mwanafunzi atatakiwa kufanya majaribio na mitihani yote ya ndani, kushindwa kufanya hivyo adhabu kali itatolewa

B.. Ikiwa mwalimu hayupo darasani mwanafunzi yampasa:-
   i. Kusoma kimya darasani.
   ii. Kutotembea ovyo darasani.
   iii. Kutotoka nje ya darasa bila sababu.

## MAADILI MEMA

A. Kila mwanafunzi wa shule hii atatakiwa
   i. Kuwahi kufika shuleni, kuheshimu walimu,wafanyakazi, viranja wa shule na wageni.
   ii. Kusimama na kusalimu wakubwa/walimu wanapopita ama kuongea nao.
   iii. Kumheshimu mwanafunzi mwenzako. Ni marufuku kabisa kuoneana hususani wanafunzi wapya. Mwanafunzi mgeni anapoonewa usisite kutoa taarifa mara moja kwa walimu au uongozi wa shule.

B. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo bila kibali.
   i. Chumba cha walimu(Staff room).
   ii. Nyumba za walimu/ wafanyakazi.

C. Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi wakati wote kwa
   i. Kuvaa nguo nzuri na vizuri.Tumbukiza shati ndani ya suruali.
   ii. Kukata nywele vizuri na kuzichana. Mitindo ya rasta, karikiti na panki hairuhusiwi. Vilevile kusuka au kunyoa vipara hakuruhusiwi.
   iii. Kunyoa ndevu, kukata kucha na kuoga kila siku.
   iv. Kutovaa mapambo kama vile mikufu, heleni, bangili, shanga, kofia, kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvaa pete n.k.

**UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE**

(i) Mwanafunzi anawajibika kutunza, na kulinda mali ya shule kwa matumizi endelevu ya wanafunzi waliopo na wale watakaokuja baadaye. Hivyo:-

- (a) Viti, madawati, meza vitunzwe mahala pake bila kuvihamisha hamisha. Ni marufuku kuburuza viti, meza au madawati.
- (b) Majembe, ndoo, kwanja, mashoka, sululu, sahani, na vikombe vitunzwe na kuwekwa mahali pake.
- (c) Madirisha na milango ya vyumba vifungwe wanafunzi wanapoondoka.
- (d) Milango na madirisha visibamizwe ovyo.

(ii) Majengo ya shule yatunzwe kwa:-

- (a) Kufagia na kudeki sakafu na kutoa buibui ukutani na madirishani.
- (b) Kusafisha madirisha na vioo
- (c) Kutoandika, kuchora na kubandika maandishi kwenye kuta
- (d) Vyoo vitumiwe na kuachwa katika hali ya usafi.

**USAJILI:**

Mwanafunzi atatumia jina lake lililoandikwa kwenye TSM 9 tu. Hairuhusiwi kubadilisha jina. Mwanafunzi atatakiwa kuonana na utawala wa shule kabla ya kuanza kutumia mali za shule.

**MUHIMU:**

- (a) Mzazi/mlezi unatakiwa kumpatia nauli mwanao ya kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
- (b) Shule haitoi chakula maalumu (special diet) kwa wagonjwa.
- (c) Nguo nyingine yoyote hairuhusiwi kuvaliwa hapa shuleni isipokuwa shamba dress na sare za shule tu.
- (d) Mzazi anashauriwa kumkatia mtoto wake bima ya Afya
- (e) Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na cassette, radio player, kisu, panga, kiberiti, bunduki, jiko, hita, chombo chochote cha muziki, mshumaa n.k.
- **(f) Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kumiliki laini ya simu, charger, simu ya mkononi katika mazingira ya shule. Akikamatwa nayo itaharibiwa kabisa na mwanafunzi atafukuzwa shule.**
- **(g) Marufuku kutoka nje ya eneo la shule bila kibali maalum toka kwa uongozi wa shule isipokuwa jumapili ya mwisho wa mwezi tu.Ukikamatwa nje ya eneo la shule bila kibali utarudishwa nyumbani kwa siku kumi na kurudi shuleni na mzazi/mlezi. Pia wazazi/walezi wanaruhusiwa kuwatembelea wanafunzi siku ya jumapili ya mwisho wa mwezi tu.**

**MICHEZO**

Michezo ni muhimu sana kwa afya. "Sound mind in a sound body", Kwa hiyo kila mwanafunzi yampasa.

(a) Kuwa na sare za michezo
(b) Kushiriki mojawapo ya michezo ya hapa shuleni
(c) Kushiriki katika mashindano ya michezo baina ya shule na timu nyingine.

**KARIBUNI SANA**

**<u>EDWARD J. MWANTIMWA</u>**
**MKUU WA SHULE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IYUNGA**

## TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili …………………………………………………………………………..

2. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………. (tarehe, mwezi mwaka)

3. Kabila…………………………. Taifa…………………………………………………

4. Dini na madhehebu………………………………………………………………...

5. jina la baba…………………………………………… Taifa…………………………

6. Anuani ya baba:…………………………………………………………………….

7. Kazi ya baba…………………………………………………………………………

8. Jina la mama:………………………………………………………………………..

9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana……………………………………..

10. Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni:-

| S/N | JINA LA MZAZI/MLEZI | UHUSIANO | SIMU NA. | ANAKOISHI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| **3** | | | | |
| 4 | | | | |

| PICHA 1 | PICHA YA 2 | PICHA YA 3 | PICHA YA 4 |
|---|---|---|---|

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (taja sehemu moja tu
Utakayokwenda kila wakati na anuani: ……………………………………………………

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi……………………………… Tarehe……………………..
Sahihi ya mzazi/mlezi………………………………. Tarehe……………………..

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS – TAMISEMI
## HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA
### SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI IYUNGA

### FOMU YA KUKUBALI

**1. Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi…………………………………………….. Ninakubali nafasi niliyopewa
Kuingia kidato cha …… mwaka……………. Katika shule ya sekondari ya Ufundi **Iyunga** na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya Elimu ya kujitegemea na sitamiliki simu ya mkononi wala kushiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni.

Anwani yangu ya kudumu ni………………………………………….
…………………………………………
…………………………………………

**2. Sehemu ya Mzazi/mlezi**

Mimi…………………………………………… ninakubali mtoto wangu
………………………………………… kuchukua nafasi kuingia Iyunga shule ya sekondari ya Ufundi kidato cha …………… mwaka ………….. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa na hatamiliki simu ya mkononi awapo shuleni wala kushiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai kwa muda wote atakapokuwa mwanafunzi.

.

Anuani yangu ya kudumu ni:

…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………
Simu Na………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Sahihi…………………………………….. Tarehe…………………

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

TO: The Medical officer
…………………………….
…………………………

From: The Headmaster
Iyunga Technical Secondary School
P.O. Box 701
MBEYA.

Date…………………………

Mr/Miss…………………………………………….. (Name in full)
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training/Secondary education. The examination should include the following Categories(1-3) each category or sub-category of which will render the applicant in eligible in case of a defect.

1. Eye-right
2. hearing
3. Limbs
4. Venereal Diseases
5. Leprosy
6. Epilepsy
7. Neuroses
8. Tuberculosis (TB)
9. Other serious diseases

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE:**
(To be completed by a Government medical Officer)

I have examined the above named and consider that he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time student (secondary education).

1. Eye sight……………………………………………………
2. Hearing…………………………………………………..
3. Limbs…………………………………………………….
4. Speech……………………………………………………
5. Venereal diseases…………………………………………
6. Leprosy……………………………………………………
7. Epilepsy…………………………………………………..
8. Neuroses…………………………………………………..
9. Tuberculosis (TB)…………………………………………...
10. Other serious diseases……………………………………

Date…………………………………………. Signature……………………….
Station…………………………………… Designation…………………….